
# ASIREGEE MOYOWE

Simon Simya






2. Bustani mle Getsemani amwomba Mungu Baba,
Je!mtu Mungu ananini nguvu zake ni haba,
Rabbi yangu waziona dhambi za binadamu,
Mwili wake umetona kama jasho la damu.

3. Salamu Rabbi salamu anena Yuda mbaya,
Mwenye moyo wake mgumu ambusu pasi haya,
Aliwaambia basi ntakaye mbusu ndiye,
Mtwaeni na kwa upesi Yuda nani ni siye.

4. Yuda nani ila yeye aliyetenda dhambi,
Akikosa kwa Munguwe mtenda dhambi haoni,
Mwenye kumtendea mema mtaka dhambi haoni,
Kwamba ni kutupa mema kumwendea shetani.

5. Wote ni kupiga mbio Mitume wepamoja,
Wamtia mikono yao askari walokuja,
Wampeleka hukumuni aamuliwe na mtu,
Mwenye kutoka uwinguni mwamzi mkuu wa watu.

6. Mtume Petro amkanusha anena simjui,
Uhodari umekwisha machoye hainui,
Pilato amwona Rabbi hakuko sataneno,
Asemasioni neno lakini nimwoga mno.

7. Hathubutu kumwachia sihukumu aomba,
Mmoja nitamfungulia Yesu au Baraba,
Wayahudi mwamtaka ni Baraba aachwe tu,
Yesu afe msalabani damuye juu yetu.

8. Pilato hukumu gani simo nanawa mkono,
Mkimtaka Yesu mwueni la mwamzi hilo neno,
Mara askari wa anza ni kupiga kelele,
Kumcheka nakumponda mwenye mema milele.